NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 24 OF 1979

I ASSENT,

Julius K. Nyerere President

.....

An Act to give statutory effect to the establishment of Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania and consequentially to disestablish the National Union of Tanganyika Workers, to repeal the National Union of Tanganyika Workers (Establishment) Act, 1964, and to provide for other matters incidental to the establishment of Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania on the fifth day of February, 1978

[.....]

WHEREAS Section 70 of the Constitution of Chama cha Mapinduzi (in this Act referred to as "the Party") provides for the establishment of organizations by and of the people united in that behalf for the performance of specific functions or for the attainment of specific objects, the affairs and activities of which organizations shall be conducted under the guidance and supervision of the Party:

AND WHEREAS, the same section 70 of the Constitution of the Party further designates the organizations to be established, including Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania:

AND WHEREAS, pursuant to that section 70 of the Constitution of the Party, there has been established Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania, which operates, and whose affairs and activities are conducted, throughout the United Republic of Tanzania:

AND WHEREAS, consequent upon the establishment of Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania, it is expedient to give statutory effect to its establishment and to make other provisions connected with the establishment of Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania, including the

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

disestablishment of the National Union of Tanganyika Workers and the repeal of the National Union of Tanganyika Workers (Establishment) Act, 1964:

Cap. 555

Now, THEREFORE, this Act is enacted by the Parliament of the United Republic of Tanzania as follows-

PART I

PRELIMINARY

Short title and construction Cap. 381

1. This Act may be cited as Jumuiya ya. Wafanyakazi wa Tanzania Act, 1979, and shall be read as one with the Trade Unions Ordinance

Commencement

2. This Act shall be deemed to have come into operation on the fifth day of February, 1978.

Interpretation

3. In this Act, unless the context requires otherwise-

"the effective date" means the fifth day of February, 1978;

"JUWATA" means Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania established pursuant to section 70 of the Constitution of the Party and referred to in the Rules;

"Minister" means the Minister for the time being responsible for labour matters;

"the Ordinance" means the Trade Unions Ordinance;

"the Party" means Chama Cha Mapinduzi;

"Registrar" means the Registrar of Trade Unions appointed under section 3 of the Ordinance, and includes an assistant registrar appointed under section 4 of the Ordinance;

"the Rules" means the Rules of JUWATA made in accordance with the provisions made in that behalf contained in the Constitution of the Party and in the Rules, as amended from time to time;

"the Union" means the National Union of Tanganyika Workers established by the National Union of Tanganyika Workers Establishment) Act, 1964.

PART II

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI WA TANZANIA

JUWATA deemed to be a union of all employees in Tanzania

4.-(1) JUWATA shall be the sole body representative of all employees within the United Republic.

(2) JUWATA shall, with effect from the effective date, be deemed to be a trade union, and the Registrar shall register it in that behalf under the Ordinance.

Membership of JUWATA

5.-(1) Subject to the Provisions of the Rules and of any other written law for the time being in force relating to the eligibility of persons to be members of trade unions, persons may become members of JUWATA in accordance with the procedure set out in the Rules, subject to sub section (2) and (3) of this section.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(2) Every person who, immediately before the effective date, was a member of the Union shall, with effect from the effective date, be deemed to have become a founder member of JUWATA, and his membership of JUWATA shall be governed by the Rules.

(3) A founder member of JUWATA shall not be liable to pay any initial fees in respect of his membership of JUWATA.

6. The Secretary-General of JUWATA, appointed in accordance with the Rules, shall be the chief executive officer of JUWATA and shall be responsible for the conduct and management of all the affairs and activities of JUWATA.

JUWATA

7.-(1) The affairs and activities of JUWATA, and their conduct and management, shall be governed by the Rules.

Rules of JUWATA

(2) For the avoidance of doubts, it is hereby declared-

(a) that the provisions of the Rules regarding the functions and powers of JUWATA, its departments, officers, organs, trustees and members shall apply to, their respective capacities only in relation to JUWATA as a trade union and nothing in the Rules shall be construed as authorizing the disregard of any enactment or rule of law by JUWATA or by any of its departments, officers, organs, trustees or members;

(b) that nothing in section 27 of the Interpretation of Laws and General Clauses Act, 1972, (which relates to the commencement and publication of subsidiary legislation), or in paragraph (e) of section 32 of that Act (which relates to the power to annex penalties to the breach of subsidiary legislation) shall apply to any of the Rules.

Acts, 1972 No. 30

(3) JUWATA shall not be deemed to be in default under any of the provisions of the Ordinance relating to the rules of a trade union and the matters to be contained in those rules, or be liable to have its registration under the Ordinance cancelled, solely by reason of the omission from the Rules of any matter required to be contained in the rules of a trade union; and nothing in section 13 (1) (f), 27 or 36 of the Ordinance shall apply to JUWATA.

(4) The Rules made in accordance with the procedure set out in the Rules may be amended, modified Or replaced in accordance with the procedure provided for in that behalf by the Rules and the provisions of the Constitution of the Party.

8.-(1) If the President is satisfied that JUWATA has failed to carry out its objects satisfactorily as a trade union or that the further operation of JUWATA as a trade union is no longer in the public interest, he of may, after obtaining the approval of the National Executive Committee of the Party, by order published in the Gazette, direct the Registrar to cancel the registration of JUWATA under the Ordinance.

President may order cancellation of registration of JUWATA as a trade union

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(2) Where the registration of JUWATA as a trade union under the Ordinance is cancelled in accordance with the provisions, of subsection (1), any new body representative of employees designated in that behalf by the Party in accordance with the provisions of section 70 of the Constitution of the Party shall, with effect from its designation, be deemed to be a trade union and shall be registered by the Registrar in that behalf under the Ordinance.

(3) Where the Registrar cancels the registration of JUWATA under the Ordinance in accordance with the provisions of subsection, (1), JUWATA shall be deemed to have been cancelled under section 14 of the Ordinance and the provisions of section 17 of the Ordinance regarding the disposal of the funds of a trade union cancelled under section 14 of the Ordinance shall apply in respect of the cancellation of JUWATA.

PART III

DISESTABLISHMENT OF THE NATIONAL UNION OF TANGANYIKA WORKERS AND INCIDENTAL PROVISIONS

Dissolution of the Union

9. The Union is disestablished and shall be deemed to have been so disestablished. as from the effective date, and the Registrar shall in that behalf cancel its registration under the Ordinance.

Transfer of assets and liabilities the Union

10.-(l) Notwithstanding the provisions of section 17 of the Ordinance, all the assets and liabilities of the Union shall, by virtue of this section of and without further assurance, be deemed to have been vested in JUWATA as from the effective date.

(2) Every person who, immediately before the effective date, was managing the affairs and business of the Union shall, upon the enactment of this Act, do all things that are necessary or desirable for the effectual vesting in accordance with the provisions of this Act of the assets and liabilities of the Union subsisting immediately before the effective date.

(3) Where before the enactment of this Act any person who, immediately before the effective date, was responsible for the management *of* the affairs and business of the Union did, or purported to do, any lawful act in relation to the assets and liabilities of the Union which if done after the enactment of this Act would have been necessary or desirable for the more effectual vesting of the assets and liabilities of the Union in JUWATA, such lawful act shall be deemed to have been done under this Act, and its performance by that person shall not be called into question in any court by reason only of that act having been done before the enactment of this Act.

Effect of dissolution of the Union

11.-(1) Every instrument specified in subsection (2) as an instrument to which that subsection applies shall, with effect from the effective date by virtue of this section, be deemed to have continued, and after the enactment of this Act shall continue, in full force and effect, -and JUWATA shall, with effect from the effective date, be deemed to have been and, after the enactment of this Act shall be-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(a) substituted for the Union as a party to the instrument;

(b) entitled to receive, and enforce payment of, any money payable under the instrument;

(c) entitled to obtain transfer, conveyance or assignment of, and enforce possession of any property which was or is to be transferred, conveyed or assigned under the instrument;

(d) liable to make payment of any money payable under the instrument;

(e) liable to transfer, convey or assign any property which was or is to be transferred, conveyed or assigned under the instrument,

as the case may be.

(2) This subsection applies to instruments (including contracts, guarantees, agreements, bonds, authorities, mortgages, charges, bills of exchange, promissory notes, bank drafts, bank cheques, letters of credit, securities, certificates of title, share and stock certificates, warrants and other documents)—

(a) to which the Union was or is a party;

(b) creating or evidencing any right of the Union to property; or under which any money was or is to be, or may have, or may become, liable to be transferred, conveyed or assigned, by the Union.

which were subsisting on or after the effective date or come into existence after the enactment of this Act.

(3) Every referrence in any written law to the Union shall be construed as a reference to JUWATA.

Legal proceedings

12.—(1) Any legal proceedings pending before any court or other tribunal which were commenced immediately before or after the effective date and to which the Union is a party may, in so far as they relate to any property, right, liability or obligation vested or deemed to have been vested in JUWATA by this Act or to any deed, bond, agreement, award or other document or instrument which, with effect from the effective date is deemed to have had or which, after the enactment of this Act, has effect in accordance with section 12, be continued by or against JUWATA.

(2) Where any proceedings were instituted by or against the Union before the enactment of this Act, in respect of any right, liability or obligation vested in the Union, JUWATA and every other party to those proceedings may take all objections and exceptions as might have been taken in proceedings by or against the Union, including any objection or exception under Part IV of the Ordinance.

Employees of the Union

13.—(1) Every person employed by the Union immediately before the effective date shall be deemed to have become employed by JUWATA as from the effective date and, as from the enactment of this Act, shall be employed by JUWATA.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(2) Where any person who, pursuant to the provisions of subsection (1), is deemed to have become an employee of JUWATA as from the effective date becomes an employee of JUWATA after the enactment of this Act, the terms and conditions of service applicable to him in his employment with JUWATA shall, except where the President directs otherwise, be not less favourable than those which were applicable to him before the effective date and, subject to any provisions of the Rules relating to officers, departments and sections of JUWATA, he shall, as from the effective date, be deemed to have been appointed to the service of JUWATA in such office as the Secretary-General of JUWATA shall determine, and for the purposes of determining any right to gratuity or other superannuation benefit, his service with JUWATA after the enactment of this Act shall be regarded as continuous with his service immediately before and after the effective date.

Validation of certain acts and proceedings

14.—(1) Where, after the effective date but before the enactment of this Act, any person who was an officer or employee of the Union immediately before the effective date purported to perform any duty or exercise any power or function imposed or conferred upon him as such officer or employee by or under any enactment or rule of law, the duty, power or function shall be deemed to have been imposed on and vested in that officer or employee as if he had been an officer or employee of JUWATA on the date on which he performed the duty or exercised the power or function, and the performance of that duty or the exercise of that power or function shall not be called in question in any court by reason only of this Act not having been enacted.

(2) Where after the effective date but before the enactment of this Act—

(a) any fees were charged and paid by any person (other than a founder member) in respect of his membership of JUWATA; or

(b) any elections were held and persons were elected to any office of JUWATA; or

(c) any appointment was made to any office of JUWATA,

in accordance with the provisions of the body of rules known as "Kanuni za Jumuiya ya Wafanyakazi" made with the approval of the Party, pursuant to section 70 (3) of the Constitution of the Party, the fees shall be deemed to have been lawfully paid, and the elections or appointments shall respectively be deemed to have been lawfully held or made under the provisions of this Act.

Repeal of Cap. 555

15. The National Union of Tanganyika Workers (Establishment) Act, 1964, is hereby repealed.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SCHEDULE

(Section 7(6))

KANUNI ZA JUMUIYA YA WAFANYAKAZI WA TANZANIA

WAJIBU WA JUMUIYA

Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania inaundwa kwa mujibu wa Sehemu ya Nne, kifungu cha 70(1) (2) (c) (3) cha Katiba ya Chama cha Mapinduzi—C.C.M. Jumuiya hii, itazingatia Imani ya CHAMA pamoja na majukumu yake kama ifuatavyo:—

(1) Kwamba Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania ndicho chombo kinachowaunganisha Wafanyakazi nchini kote katika hali yao ya Wafanyakazi.

(2) Kwamba katika nchi inayojenga Ujamaa kama Tanzania na ambayo imekwisha chukua hatua muhimu za kuweka njia kuu za uchumi chini ya Serikali kwa kupitia vyombo mbali mbali vya umma, jukumu la awali la Jumuiya ya Wafanyakazi ni kuhakikisha kuwa madaraka ya nchi yanabaki na kuthibitiwa barabara na CHAMA.

(3) Kwamba jukumu muhimu la Wafanyakazi katika kipindi cha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kijamaa ni kuongeza uzalishaji mali na utanuzi wa shughuli za kijamaa ili kutosheleza mahitaji ya maendeleo ya Wakulima na Wafanyakazi na ya Uchumi wa Taifa hatua kwa hatua.

(4) Kwamba katika nchi inayojenga Ujamaa kama Tanzania jukumu la kutawala ni la tabaka la Wafanyakazi na la Wakulima chini ya uongozi wa CHAMA.

(5) Kwamba Wafanyakazi wanayo maslahi yao ambayo lazima yazingatiwe, yatetewe, yaendelezwe lakini kwa uwiano na maslahi ya Wakulima ambao pamoja na Wafanyakazi ndio msingi wa Taifa letu na chimbuko la siasa yetu ya Kijamaa na Kujitegemea.

(6) Kwamba Jumuiya ya Wafanyakazi katika nchi ya Kijamaa ni chombo cha mapambano dhidi ya ubepari, umwinyi na tabia zote za uzembe, utegaji, uvivu, ulevi zilizo kinyume na hisia na nidhamu ya kimapinduzi ya kifanyakazi.

(7) Kwamba Jumuiya ya Wafanyakazi ni chombo cha kushirikisha Wafanyakazi kikamilifu katika kujenga, kuendeleza na kuimarisha Jumuiya ya Wafanyakazi wa Afrika. Jumuiya yaWafanyakazi itakuwa na jukumu la kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi na Mashirika ya Kimataifa yanayojishughulisha na maendeleo ya wafanyakazi kutoka katika hali ya kunyonywa ili mradi Vyama na Mashirika haya yanaamini Uhuru, Usawa na Haki za Binadamu.

Kwa hiyo basi wajibu wa Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania utakuwa:—

(a) Kuifikisha siasa ya CHAMA kwa kila mfanyakazi na kuhakikisha kwamba maagizo ya CHAMA yanatekelczwa kwa upande wa Wafanyakazi.

(b) Kulinda siasa ya CHAMA dhidi ya wapinga Ujamaa wa aina zote katika sehemu za kazi na nchini kwa jumla.

(c) Kujenga na kudumisha juhudi, ari ya kazi, nidhamu na mwamko wa kifanyakazi miongoni mwa wafanyakazi.

(d) Kueneza elimu ya Wafanyakazi na mapinduzi ya kiufundi kwa Wafanyakazi na Wakulima kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali vinavyohusika.

(e) Kuhakikisha kwamba Wafanyakazi wanatekeleza wajibu wao wa kutimiza malengo ya uzalishaji mali na ya huduma yaliyokubaliwa.

(f) Kuhakikisha kwamba Wafanyakazi popote walipo wanashiriki katika kuendesha na kusimamia mwenendo wa uchumi ikizingatiwa kuwa nchi ya Ujamaa ni ya Wakulima na Wafanyakazi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(g) Kuujenga moyo wa kujiamini miongoni mwa Wafanyakazi jambo amba likikosekana utekelezaji wa kifungu (f) hauwezekani.

(h) Kushirikiana na Serikali kuona kwamba huduma muhimu kama vile matibabu vituo vya mapumziko ya wafanyakazi, n.k., wanapatiwa Wafanyakazi.

(i) Kuendeleza heshima, haki na maslahi ya wafanyakazi na kushiriki katika kuweka siasa ya mishahara na maslahi ya wafanyakazi kwa jumla.

(j) Chombo cha CHAMA cha kuhakikisha kwamba kila Mfanyakazi atalipwa kwa kadri ya kazi yake, kwamba kima cha chini cha mshahara kilichowekwa kisheria kinaheshimiwa na kwamba mfanyakazi popote alipo hanyanyaswi na mwajiri yoyote.

SEHEMU YA KWANZA

Jina

1. Jina la Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania litakuwa "JUMUIYA YA WAFANYAKAZI WA TANZANIA", kwa kifupi "JUWATA".

Makao Makuu

2. Makao Makuu ya Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania yatakuwa DODOMA.

SEHEMU YA PILI

Uwanachama

3.—(a) Wafanyakazi waliokuwa wanachama wa NUTA kabla ya kuvunjwa kwa Umoja huo watakuwa wanachama waanzilishi wa JUWATA isipokuwa kama watakataa wenyewe.

(b) Mfanyakazi yeyote mwajiriwa anayeishi Tanzania ambaye sheria ya nchi haimzuii kufanya hivyo anayo haki ya kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Wafanyakazi.

(c) Mfanyakazi anayetaka kujiunga na Jumuiya ya Wafanyakazi atapeleka ombi lake kwa Katibu wa JUWATA wa Tawi lake la kazi. Ombi lake laweza kukubaliwa au kukataliwa na Kamati ya JUWATA ya Tawi. Pindi akikubaliwa atalipa kiingilio na Ada na kupewa Kadi.

Kiingilio

4.—(a) Kiingilio cha Mfanyakazi kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Wafanyakazi kitakuwa Sh. 5/-.

Ada

(b) Wanachama wa JUWATA wanaopata mishahara kuanzia kima cha chini mpaka Sh. 700/- kwa mwezi watalipa ada ya Sh. 3/- kila mwezi.

(c) Wanachama wa JUWATA wanaopata mishahara zaidi ya Sh. 700/- kwa mwezi watalipa Sh. 6/- kila mwezi.

(d) Ada hizo zitaweza kubadilika kutokana na uamuzi na maazimio ya Mkutano Mkuu wa JUWATA.

Kutoka katika Umoja

5.—(a) Mfanyakazi ataacha kuwa Mwanachama wa Jumuiya ya Wafanyakazi kwa:—

(i) Kujiuzulu mwenyewe; au

(ii) Kuachishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi; au

(iii) Kukoma kuwa mfanyakazi wa kuajiriwa; au

(iv) Kutolipa ada yake ya kila mwezi kwa muda wa miezi sita au zaidi bila ya sababu ya kuridhisha. Isipokuwa kama atakuwa tayari kulipa mali mbikizo ya ada hiyo.

(b) Mfanyakazi ambaye ametoka katika Jumuiya ya Wafanyakazi hatarudishiwa kiingilio wala ada zozote alizotoa, isipokuwa faida zozote zilizopatikana chini ya mpango wa akiba ulioanzishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi wakati alipokuwa katika Jumuiya hii.

Wajibu wa Mfanyakazi

6. Kila Mfanyakazi atakuwa na wajibu ufuatao:—

(a) Kutimiza wajibu wake wa kazi kwa juhudi na maarifa na kuwa mkweli na mwaminifu daima.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(b) Kupiga vita uvivu, uzembe, ulevi na aina nyingine zote za tabia mbaya kazini.

(c) Kujielimisha kwa uwezo wake wote na kutumia elimu hiyo kwa faida ya Wafanyakazi wenzake wa Taifa.

(d) Kutekeleza kwa hali ya juu maazimio mbali mbali yatakayopitishwa na vikao vya Jumuiya hii kwa misingi ya CHAMA.

Haki za Mwanachama

7. Mfanyakazi mwanachama wa JUWATA atakuwa na haki zifuatazo:—

(a) Haki ya kuchagua viongozi wake wa Jumuiya na haki ya kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Jumuiya kwa mujibu wa Kanuni na Sheria au Taratibu za Wafanyakazi.

(b) Haki ya kujitetea au kutoa maelezo yake mbele ya kikao cha JUWATA kinachohusika katika mashitaka yoyote yaliyotolewa juu yake, pamoja na haki ya kukata rufani ya kwenda katika kikao cha juu zaidi cha JUWATA kama kipo endapo hakuridhika na uamuzi uliotolewa.

(c) Haki ya kutetewa na Jumuiya ya Wafanyakazi kuhusu haki na maslahi yake yanayohusu kazi yake kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa.

(d) Haki ya kufaidi matunda yatokanayo na shughuli za kiuchumi na Ustawi wa Jamii zinazoendeshwa na Jumuiya kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Sehemu za Kazi za Jumuiya

8.—(a) Kutakuwa na sehemu na vijisehemu vifuatavyo katika Jumuiya ya Wafanyakazi:—

(i) WAFANYAKAZI VIWANDANI NA MIGODI:
Visehemu vyake vitakuwa:
(1) Wafanyakazi Viwandani;
(2) Wafanyakazi migodini na machimbo ya mawe.

(ii) WAFANYAKAZI WA BIASHARA, USAFIRISHAJI NA UJENZI:
Visehemu vyake vitakuwa:
(1) Wafanyakazi katika shughuli za Biashara;
(2) Wafanyakazi katika shughuli za Usafirishaji;
(3) Wafanyakazi katika shughuli za Ujenzi.

(iii) WAFANYAKAZI WA KAZI ZA JUMLA KATIKA IDARA AU TAASISI MBALI MBALI:
Visehemu vyake ni:
(1) Ushuru na Forodha;
(2) Idara ya Utabiri wa Hewa;
(3) Idara ya Uongozi wa Ndege;
(4) Makao Makuu na Vituo vya Utafiti.

(iv) WAFANYAKAZI WA RELI:
Visehemu vyake ni:
(1) Reli ya Shirika la Reli la Tanzania;
(2) Reli ya Uhuru (TAZARA).

(v) WAFANYAKAZI WA MASHIRIKA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:
Visehemu vyake ni:
(1) Wafanyakazi wa Shirika la Posta na Simu za Nje;
(2) Wafanyakazi wa Shirika la Ndege;
(3) Wafanyakazi wa Shirika la Bandari;
(4) Wafanyakazi wa Shughuli za kupakia na kupakua mizigo Bandarini

(vi) WAFANYAKAZI WA SERIKALI NA WAGANGA:
Visehemu vyake ni:

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(1) Wafanyakazi Serikalini;

(2) Waganga.

(vii) SEHEMU YA WALIMU:

Sehemu itakuwa na kisehemu kimoja tu cha walimu.

(viii) WAFANYAKAZI WAAJIRIWA KATIKA MASHAMBA YA UMMA NA YA BINAFSI:

Sehemu hii itakuwa na kisehemu kimoja tu cha Kilimo.

(ix) WAFANYAKAZI WA KAZI MAHOTELINI, MAJUMBANI NA KAZI NYINGINEZO:

Visehemu vyake ni:

(1) Wafanyakazi Mahotelini na Majumbani;

(2) Wafanyakazi nyinginezo kwa mfano, Madobi, Vinyozi na wengineo ambao hawakutajwa katika sehemu nyingine.

(b) Baraza Kuu la JUWATA lina uwezo wa kufunga sehemu yo yote ya kazi au kuanzisha sehemu moja kuwa sehemu mbili au zaidi baada ya kupata idhini ya CHAMA.

(c) Wanachama wa JUWATA wanaomba nafasi za uongozi katika ngazi mbali mbali za sehemu za kazi watafikiriwa na Kamati za Tawi za ngazi mbali mbali zinazohusika na Umoja wa Wafanyakazi kama inavyoonyeshwa katika Kanuni hizi.

(d) Shughuli zote za sehemu hizi za Umoja wa Wafanyakazi zitakuwa chini ya uongozi wa Baraza Kuu la Jumuiya ya Wafanyakazi.

SEHEMU YA TATU

VIKAO VYA JUMUIYA YA WAFANYAKAZI:—FUNGU LA I

Tawi

9. Kikao cha kwanza kabisa cha Jumuiya ya Wafanyakazi kitakuwa Tawi:—

(a) Kwa kibali cha JUWATA Wilayani, Jumuiya ya Wafanyakazi itaanzisha Tawi mahali pa kazi penye wanachama wa JUWATA wasiopungua kumi.

(b) Iwapo patakuwapo mahali pa kazi pasipokuwa na wanachama waliotimu kumi, Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya inaweza kuunganisha wanachama hao pamoja na wanachama wengine wa hali hiyo ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za Jumuiya.

(c) Kila Tawi litaandikishwa katika Makao Makuu ya Jumuiya ya Wafanyakazi.

Vikao vya Matawi

10. Kutakuwa na Vikao vifuatavyo vya Jumuiya ya Wafanyakazi katika kila Tawi:—

(a) Mkutano wa Wafanyakazi wote wa Tawi;

(b) Mkutano wa Mwaka wa Tawi;

(c) Kamati ya Tawi.

Mkutano wa Wafanyakazi

11.—(a) Kutakuwa na Mkutano wa Wafanyakazi wote kwa kila Tawi;

(b) Mkutano huu utazungumzia mambo yote yanayohusu utekelezaji wa kazi na maendeleo ya wafanyakazi wa Tawi na Taifa;

(c) Mkutano wa wafanyakazi wote utafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila baada ya miezi minne, lakini unaweza kufanyika wakati wo wote iwapo utaitishwa na Kamati ya Tawi.

(d) Mwenyekiti wa Tawi ndiye atakayekuwa Mwenyekiti wa Mikutano hii. Kama hayupo Mwanachama wa JUWATA miongoni mwao anaweza kuchaguliwa na kikao kuwa Mwenyekiti wa Mkutano.

Mkutano wa Mwaka wa Tawi

12. Kutakuwa na Mkutano wa Mwaka wa Tawi ambao utakuwa na Wajumbe wafuatao:—

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;
(b) Katibu wa JUWATA;
(c) Wajumbe wote wa Kamati ya Tawi;
(d) Wanachama wote wa Tawi wa Jumuiya ya Wafanyakazi katika Tawi;
(e) Katibu wa CHAMA wa Tawi;
(f) Mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya ya CHAMA;
(g) Kamisaa wa CHAMA.

Kazi za Mkutano wa Mwaka wa Tawi

13.—(a) Mkutano wa Tawi ndicho kikao kikuu cha Jumuiya ya Wafanyakazi katika Tawi;

(b) Utafikiria na kupokea taarifa ya kazi za Jumuiya katika Tawi iliyotolewa na Kamati ya Tawi na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa kipindi kijacho;

(c) Utapokea na kufikiri maazimio ya vikao vya juu vya Jumuiya ya Wafanyakazi na kutoa maelekezo kwa Kamati ya Tawi.

(d) Utakapofika wakati wa uchaguzi Mkutano utafanya yafuatayo:—

(i) Utamchagua Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi;

(ii) Utamchagua Katibu wa JUWATA wa Tawi;

(iii) Utachagua Wajumbe wa Kamati ya Tawi kwa utaratibu wa Kanuni hizi kuhusu Wajumbe wa Kamati ya Tawi;

(iv) Utachagua Wajumbe watatu wa Mkutano Mkuu wa CHAMA wa Tawi;

(v) Utachagua Mjumbe mmoja mmoja wa Vikao vya Tawi vya Jumuiya nyingine za CHAMA;

(e) Unaweza kuunda Kamati ndogo ndogo kwa utekelezaji ulio bora zaidi wa shughuli za Jumuiya ya Wafanyakazi.

(f) Mkutano huu utafanyika mara moja kwa mwaka. Lakini unaweza kufanyika wakati wo wote ukiitwa na Kamati ya Tawi.

(g) Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi ndiye atakayekuwa Mwenyekiti wa mikutano hii. Kama hayupo Mjumbe mwingine miongoni mwao anaweza kuchaguliwa na kuongoza Mkutano huu.

Kamati ya Tawi

14. Kutakuwa na Kamati ya Tawi kwa kila Tawi ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(i) Wajumbe wa tano (pamoja na Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi na Katibu wa JUWATA wa Tawi) kama idadi ya wanachama wa Jumuiya haizidi hamsini; au

(ii) Wajumbe kumi (pamoja na Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi na Katibu wa JUWATA wa Tawi) kama idadi ya wanachama wa Jumuiya inazidi hamsini lakini haizidi mia moja; au

Wajumbe kumi na tano (pamoja na Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi na Katibu wa JUWATA wa Tawi) kama idadi ya wanachama wa Jumuiya inazidi mia moja lakini haizidi elfu moja; au

Wajumbe ishirini (pamoja na Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi na Katibu wa JUWATA wa Tawi) kama idadi ya wanachama wa Jumuiya inazidi elfu moja;

(iii) Wajumbe wa Halmashauri ya Jumuiya ya Wafanyakazi ya Wilaya waliomo katika Tawi hilo.

(iv) Katibu wa CHAMA wa Tawi.

Kazi za Kamati ya Tawi

15. Kazi za Kamati ya kila Tawi zitakuwa zifuatazo:—

(a) Kuandaa Wafanyakazi kuinua ufanisi wa kazi;

(b) Kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya Elimu ya Wafanyakazi mahali pa kazi;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(c) Kuona kwamba Wafanyakazi na Waajiri wanatimiza wajibu wao wa kuzalisha mali kwa kutimiza malengo na wa kulinda Uchumi wa Nchi;

(d) Kujenga na kudumisha Jumuiya ya Wafanyakazi katika mahali pa kazi;

(e) Kudumisha ushirikiano kati ya Wafanyakazi na viongozi wa kazi;

(f) Kupanga, kudhibiti na kusimamia mapato na matumizi ya Jumuiya ya Wafanyakazi katika Tawi;

(g) Kamati ya Tawi itafanya mikutano yake si chini ya mara moja kwa mwezi. Lakini inaweza kufanya mikutano siyo ya kawaida wakati wowote ikiitishwa na Katibu wa JUWATA wa Tawi akishauriana na Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi;

(h) Mwenyekiti wa Kamati ya Tawi ni Mwenyekiti wa JUWATA wa Tawi. Kama hayupo Mjumbe mwingine miongoni mwao atachaguliwa kuongoza kikao

Viongozi Matawi

16. Kutakuwa na Viongozi wafuatao katika kila Tawi:—

(a) Mwenyekiti na Katibu wa JUWATA watakuwa Wajumbe katika Halmashauri ya CHAMA ya Tawi.

Katibu

17. Katibu wa JUWATA wa Tawi:—

(a) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi katika Tawi. Atafanya kazi zake chini ya uongozi wa Kamati ya Tawi.

(b) Kwa kushauriana na Mwenyekiti wake atakuwa na wajibu wa kuitisha Mikutano yote ya vikao vya Tawi;

(c) Atatunza fedha na kumbukumbu zote za Tawi.

FUNGU LA II.—VIKAO VYA WILAYA

Vikao vya Wilaya

18. Kutakuwa na vikao vifuatavyo katika kila Wilaya:—

(a) Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya;

(b) Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya.

Halmashauri ya JUWATA

19. Kutakuwa na Halmashauri ya JUWATA kwa kila Wilaya ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;

(b) Katibu wa JUWATA;

(c) Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya;

(d) Wajumbe waliochaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Kamati za matawi ili kwamba kila kisehemu cha sehemu ya kazi kilichopo Wilayani kiwe kinawakilishwa na wajumbe wawili;

(e) Mjumbe wa Halmashauri ya JUWATA ya Mkoa aliyepo katika Wilaya hiyo;

(f) Katibu wa CHAMA wa Wilaya;

(g) Mjumbe mmoja kutoka katika kila Jumuiya ya CHAMA.

Kazi za Halmashauri

20.—(a) Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya ndicho kikao kikuu cha kuzungumzia malengo ya shughuli za Wafanyakazi katika Wilaya;

(b) Itapokea na kutekeleza maazimio ya vikao vya juu ya Jumuiya ya Wafanyakazi

(c) Itazungumzia mambo yote yanayohusu maendeleo ya Wafanyakazi kwa Wilaya hiyo;

(d) Inaweza kuunda Kamati ndogo ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa siasa na shughuli za maendeleo ya Wafanyakazi Wilayani;

(e) Unapofika wakati wa uchaguzi Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya itafanya yafuatayo:—

(i) Itachagua Mwenyekiti wa JUWATA wa Wilaya;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Itachagua Wajumbe wa Baraza la JUWATA la Mkoa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Halmashauri ya Wilaya hivyo kwamba kila kisehemu cha kazi katika Wilaya hiyo kiwe na mjumbe mmoja;

(iii) Itachagua Mjumbe mmoja wa Mkutano Mkuu wa JUWATA;

(iv) Itachagua Wajumbe watatu wa Mkutano Mkuu wa CHAMA wa Wilaya

(v) Itachagua Mjumbe mmoja mmoja wa vikao vya Wilaya vya Jumuiya zingine za CHAMA;

(vi) Itachagua Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya mmoja mmoja kutoka kila sehemu ya kazi ya JUWATA Wilayani;

(f) Halmashauri itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kwa mwaka wakati wo wote iwapo itaagizwa kufanya hivyo na Halmashauri ya JUWATA ya Mkoa au kikao kingine cha juu;

(g) Mwenyekiti wa JUWATA wa Wilaya ataongoza mikutano yote ya Halmashauri hii lakini kama hayupo Mjumbe mwingine miongoni mwao atachaguliwa kuongoza mkutano huo.

Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya

21. Kutakuwa na Kamati ya Utekelezaji kwa kila Wilaya ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(i) Mwenyekiti wa JUWATA;

(ii) Katibu wa JUWATA;

(iii) Mjumbe mmoja kutoka kila sehemu ya Wafanyakazi iliyopo Wilayani.

Kazi za Kamati ya Utekelezaji

22. Kazi za Kamati za Utekelezaji za Wilaya zitakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kusimamia na kuongoza kazi za kila siku za Jumuiya ya Wafanyakazi Wilayani;

(b) Kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Jumuiya ya Wafanyakazi Wilayani;

(c) Kuona kwamba Wafanyakazi wanatimiza wajibu wao wa kuzalisha mali au kutoa huduma kwa kutimiza na kupindukia malengo yaliyowekwa na kwamba wanalinda na kuhifadhi Uchumi wa Nchi;

(d) Itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Utendaji ya CHAMA ya Wilaya majina ya wanaoomba nafasi za uongozi katika Jumuiya ya Wafanyakazi Wilayani;

(e) Kupanga na kudhibiti mapato na matumizi ya Jumuiya ya Wafanyakzi Wilayani;

(f) Itaandaa mikutano yote ya Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya;

(g) Kamati ya Utekelezaji itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kwa miezi minne lakini mkutano usiokuwa wa kawaida unaweza kuitishwa wakati wo wote na Katibu akishauriana na Mwenyekiti;

(h) Mwenyekiti wa JUWATA wa Wilaya ataongoza mikutano yote ya Kamati hii lakini kama hayupo Mjumbe mwingine miongoni mwao atachaguliwa kuongoza mkutano huo.

Viongozi wa Wilaya

23. Kutakuwa na viongozi wafuatao katika kila Wilaya:—

(i) Mwenyekiti wa JUWATA;

(ii) Katibu wa JUWATA.

Mwenyekiti na Katibu watakuwa Wajumbe katika Halmashauri Kuu ya CHAMA ya Wilaya.

Katibu

24.—(a) Atateuliwa na Kamati Kuu ya CHAMA na atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi katika Wilaya, atafanya kazi zake chini ya uongozi wa Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya.

(b) Atakuwa na wajibu wa kuitisha mikutano yote ya JUWATA Wilayani kwa kushauriana na Mwenyekiti.

(c) Atatunza fedha na kumbukumbu za Jumuiya ya Wafanyakazi katika Wilaya.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

FUNGU LA III.—VIKAO VYA MKOA

Vikao vya Mkoa

25. Kutakuwa na vikao vifuatavyo vya Jumuiya ya Wafanyakazi katika kila Mkoa:—

(a) Baraza la JUWATA la Mkoa;

(b) Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa.

Baraza la JUWATA

26. Kutakuwa na Baraza la JUWATA la Mkoa kwa kila Mkoa ambalo litakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(i) Mwenyekiti wa JUWATA;

(ii) Katibu wa JUWATA;

(iii) Wajumbe kutoka Wilayani waliochaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 20 (e) (ii);

(iv) Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa;

(v) Mwenyekiti wa JUWATA wa Wilaya waliomo Mkoani;

(vi) Makatibu wa JUWATA wa Wilaya waliomo Mkoani;

(vii) Katibu wa CHAMA wa Mkoa;

(viii) Mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya za CHAMA.

Kazi za Baraza

27.—(a) Litasimamia utekelezaji wa shughuli zote za Jumuiya ya Wafanyakazi Mkoani;

(b) Litapokea na kutekeleza maazimio ya vikao vya juu vya Umoja wa Wafanyakazi;

(c) Kitapokea taarifa ya shughuli zilizofanywa na Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa na kutoa maelekezo kwa Kamati hiyo;

(d) Litazungumzia mambo yote ya maendeleo ya Wafanyakazi ya Mkoa;

(e) Linaweza kuunda Kamati ndogo ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za maendeleo ya Wafanyakazi katika Mkoa;

(f) Unapofika wakati wa uchaguzi Baraza la JUWATA la Mkoa litafanya yafuatayo:—

(i) Litachagua Mwenyekiti wa JUWATA wa Mkoa;

(ii) Litachagua Mjumbe mmoja wa Mkutano Mkuu wa CHAMA wa Taifa;

(iii) Litachagua wajumbe watatu wa Mkutano Mkuu wa CHAMA wa Mkoa;

(iv) Litachagua wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa, Mjumbe mmoja mmoja kutoka kila sehemu ya kazi za Wafanyakazi zilizopo katika Wilaya za Mkoa huo.

(v) Litachagua mjumbe mmoja mmoja wa vikao vya Mkoa vya Jumuiya nyingine za CHAMA.

(g) Baraza litafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kwa mwaka, lakini linaweza kufanya mkutano wakati wo wote mwingine iwapo litaagiza kufanya hivyo na kikao kingine cho chote cha juu au likiitishwa na Kamati ya Utekelezaji ya JUWATA ya Mkoa;

(h) Mwenyekiti wa JUWATA wa Mkoa ataongoza mikutano ya Baraza hili lakini kama hayupo mjumbe mwingine miongoni mwao atachaguliwa kuongoza mkutano huo.

Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa

28. Kutakuwa na Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa kwa kila Mkoa ambao utakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;

(b) Katibu wa JUWATA;

(c) Mjumbe mmoja mmoja kutoka kila sehemu ya kazi za Wafanyakazi zilizoko katika kila Wilaya waliochaguliwa na Baraza la JUWATA la Mkoa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

29.—(a) Kusimamia na kuongoza kazi za kila siku za Jumuiya ya Wafanyakazi; Mkoani; Kazi za Kamati

(b) Kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Jumuiya ya Wafanyakazi Mkoani

(c) Kuona kwamba Wafanyakazi na Waajiri wanatimiza wajibu wao wa kuzalisha mali kwa kutimiza malengo na wa kulinda Uchumi wa Nchi;

(d) Kupanga, kudhibiti mapato na matumizi ya Jumuiya ya Wafanyakazi katika Mkoa;

(e) Itafikiria na kutoa mapendekezo yake juu ya wanachama wa JUWATA wanaoomba nafasi za uongozi katika uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya ya Wafanyakazi wa Mkoa na kuyapeleka katika Kamati ya Utendaji ya CHAMA ya Mkoa.

30. Kutakuwa na viongozi wafuatao katika kila Mkoa:— Viongozi wa Mkoa

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;

(b) Katibu wa JUWATA.

Mwenyekiti na Katibu wa JUWATA watakuwa Wajumbe katika Halmashauri Kuu ya CHAMA ya Mkoa.

31.—(a) Atateuliwa na Kamati Kuu ya CHAMA na atakuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Jumuiya ya Wafanyakazi katika Mkoa na atafanya kazi zake chini ya uongozi wa Baraza la JUWATA la Mkoa; Katibu

(b) Atakuwa na wajibu wa kuitisha mikutano yote ya vikao vya Mkoa kwa kushauriana na Mwenyekiti;

(c) Atatunza fedha na kumbukumbu za Umoja wa Wafanyakazi katika Mikoa.

FUNGU LA IV

Vikao Vikuu Vya Jumuiya Ya Wafanyakazi

32. Kutakuwa na Vikao Vikuu vya Jumuiya ya Wafanyakazi vifuatavyo:— Vikao Vikuu

(a) Mkutano Mkuu wa JUWATA;

(b) Baraza Kuu la JUWATA;

(c) Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu.

33. Mkutano Mkuu utakuwa na Wajumbe wafuatao:— Mkutano Mkuu

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;

(b) Katibu Mkuu wa JUWATA;

(c) Wajumbe wa Baraza Kuu la JUWATA;

(d) Wenyeviti wa JUWATA wa Wilaya;

(e) Makatibu wa JUWATA wa Wilaya;

(f) Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa JUWATA waliochaguliwa na Halmashauri ya JUWATA ya Wilaya;

(g) Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CHAMA wa Taifa, mmoja kutoka kila Mkoa aliyechaguliwa na Baraza la JUWATA la Mkoa;

(h) Katibu Mtendaji Mkuu wa CHAMA;

(i) Mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya ya CHAMA;

(j) Mjumbe anayehudhuria vikao vikuu vya Jumuiya nyingine za CHAMA.

34.—(a) Mkutano Mkuu atukuwa ndicho kikao cha juu kupita vyote katika Jumuiya ya Wafanyakazi; Kazi za Mkutano Mkuu

(b) Utapokea na kujadili taarifa ya kazi za Jumuiya ya Wafanyakazi kama zilivyoletwa na Baraza Kuu;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(c) Utaweka mipango itakavyoongoza shughuli zote za Jumuiya ya Wafanyakazi;

(d) Utakuwa na uwezo wa kubadili sehemu yo yote ya Kanuni za Jumuiya ya Wafanyakazi kwa uamuzi wa theluthi mbili za Wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Tanzania Visiwani. Mabadiliko haya hayana budi yathibitishwe na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama kabla ya kutumika;

(e) Unaweza kuunda Kamati ndogo ndogo kama onaona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora zaidi wa shughuli za maendeleo ya Wafanyakazi;

(f) Utakapofika wakati wa uchaguzi Mkutano Mkuu utashughulikia mambo yafuatayo:—

(i) Utamchagua Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyakazi;

(ii) Utachagua idadi sawa ya Wajumbe wa Baraza Kuu; Wajumbe kumi kutoka Tanzania Bara na Wajumbe kumi kutoka Tanzania Visiwani, kwa utaratibu uliokubaliwa na CHAMA;

(iii) Utachagua Mjumbe mmoja mmoja wa vikao vikuu vya Jumuiya nyingine za CHAMA.

(g) Mkutano Mkuu utakutana mara moja kila baada ya miaka mitatu;

(h) Mwenyekiti wa JUWATA ndiye atakayekuwa Mwenyekiti wa kikao lakini kama hayupo mkutano unaweza kumchagua Mjumbe mwingine wa mkutano kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

Baraza Kuu

35.—(1) Kutakuwa na Baraza Kuu la Jumuiya ya Wafanyakazi;

(2) Baraza Kuu litakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;

(b) Katibu Mkuu wa JUWATA;

(c) Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu;

(d) Wenyeviti wa JUWATA wa Mikoa;

(e) Makatibu wa JUWATA wa Mikoa;

(f) Wajumbe wa Baraza Kuu, kumi kutoka Tanzania Bara na kumi kutoka Tanzania Visiwani waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa JUWATA;

(g) Katibu Mtendaji Mkuu wa CHAMA;

(h) Mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya ya CHAMA;

(i) Mjumbe mmoja kutoka kila sehemu ya Wafanyakazi katika kila mkoa.

Kazi za Baraza Kuu

36. Kazi za Baraza Kuu la Jumuiya ya Wafanyakazi zitakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Litakuwa ndilo Baraza Kuu la kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wafanyakazi kwa jumla;

(b) Litatayarisha na kuandaaa Mkutano Mkuu wa JUWATA;

(c) Litapokea kujadili taarifa ya Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu;

(d) Litajadili mapato, matumizi na makadirio ya mwaka ya fedha za Umoja wa Wafanyakazi kabla ya kuyafikisha katika Kamati Kuu ya CHAMA kupata kibali;

(e) Baraza Kuu linaweza kuunda shughuli za kiuchumi chini ya Shirika maalum litakalokubaliwa na CHAMA litakalokuwa chini ya Baraza Kuu ili kusaidia na kuinua uchumi na maendeleo ya Wafanyakazi;

(f) Litakuwa na uwezo wa kumwachisha kiongozi yeyote wa Umoja wa Wafanyakazi isipokuwa wale walioteuliwa na CHAMA;

(g) Litakuwa na uwezo wa kumwondoa katika uwanachama wa JUWATA mfanyakazi anayekiuka taratibu na Kanuni za Jumuiya ya Wafanyakazi;

(h) Kupokea, kuyafikiria na kukubali au kukataa maombi ya Mfanyakazi aliyejiunga katika Jumuiya hii aliyeachishwa uwanachama wa JUWATA ambaye anataka tena kujiunga na Jumuiya ya Wafanyakazi;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(i) Litazungumzia masuala yote yanayohusu mashirikiano ya Wafanyakazi wa Tanzania na Wafanyakazi wa nchi nyingine wanaojishughulisha na maendeleo ya ukombozi wa mfanyakazi;

(j) Unapofikia wakati wa uchaguzi Baraza Kuu litashughulikia yafuatayo:—

(i) Litachagua wajumbe saba wa Baraza la Wadhamini la Jumuiya ya Wafanyakazi;

(ii) Litachagua wajumbe kumi wa Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu, watano kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Tanzania Visiwani kwa utaratibu uliokubaliwa na CHAMA;

(iii) Litachagua wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu mmoja mmoja kutoka kila sehemu ya kazi za Jumuiya hii;

(k) Litakuwa na uwezo wa kujaza nafasi yoyote itakayotokea ya Wajumbe wake mpaka hapo Mkutano Mkuu utakapokutana na kufanya uchaguzi mwingine;

(l) Baraza Kuu litaweka utaratibu wa kutatuwa migogoro kuhusu kila sehemu ya kazi;

(m) Baraza Kuu litakutana si chini ya mara moja kwa mwaka. Lakini linaweza kukutana wakati wowote ikibidi;

(n) Mwenyekiti wa mikutano yote ya Baraza Kuu atakuwa Mwenyekiti wa JUWATA kama hayupo Mjumbe mwingine miongoni mwao atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu

37.—(a) Kutakuwa na Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu;

(b) Kamati hii itakuwa na Wajumbe wafuatao:—

(i) Mwenyekiti wa JUWATA;

(ii) Katibu Mkuu wa JUWATA;

(iii) Mjumbe mmoja mmoja kutoka kila sehemu ya kazi za Jumuiya hii aliyechaguliwa na Baraza Kuu;

(iv) Wajumbe kumi waliochaguliwa na Baraza Kuu, watano kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Tanzania Visiwani.

Kazi za Kamati ya Usimamizi

38. Kazi za Kamati ya usimamizi ya Baraza Kuu zitakuwa kama zifuatazo:—

(a) Itasimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya juu;

(b) Itasimamia chombo au vyombo vya Uchumi vya Jumuiya;

(c) Itasimamia shughuli zote za matumizi ya fedha za Jumuiya;

(d) Itaunda Kamati Maalum ya Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu ili kusimamia shughuli zote za Jumuiya kwa Tanzania Visiwani. Kamati hii itafanya kazi chini ya Kamati ya Usimamizi ya Baraza Kuu;

(e) Itaweza kuunda Kamati ndogo ndogo kama inavyoona inafaa kwa utekelezaji bora wa shughuli za Wafanyakazi;

(f) Itafikiria na kupendekeza majina ya wanachama wa JUWATA wanaoomba nafasi za uongozi wa vikao vya juu ya JUWATA na kupeleka mapendekezo yake kwenye Kamati Kuu ya CHAMA;

(g) Itafikiria na kupendekeza majina ya Wafanyakazi na Wakulima wanaoomba nafasi za uongozi katika uchaguzi wa Bunge la Tanzania na kupeleka mapendekezo yake katika Kamati Kuu ya CHAMA;

(h) Itakuwa na uwezo wa kumwachisha au kumwondoa kazi Mtendaji ye yote isipokuwa yule aliyeteuliwa na CHAMA katika ngazi ya Taifa;

(i) Inaweza kuunda Idara mbali mbali katika Ofisi Kuu kama inavyoona inafaa baada ya kukubaliwa na Baraza Kuu;

(j) Itakutana si chini ya mara moja kila baada ya miezi mitatu, lakini inaweza kufanya mkutano usio wa kawaida wakati wo wote ikibidi;

(k) Mwenyekiti wa JUWATA atakuwa Mwenyekiti wa mikutano ya Kamati. Kama hayupo Kamati itachagua Mjumbe mwingine miongoni mwake kuongoza mkutano huu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Viongozi Wakuu

39. Jumuiya ya Wafanyakazi itakuwa na Viongozi wakuu wafuatao:—

(a) Mwenyekiti wa JUWATA;

(b) Katibu Mkuu wa JUWATA.

Mwenyekiti na Katibu Mkuu watakuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CHAMA.

SEHEMU YA NNE

WATENDAJI WA JUMUIYA YA WAFANYAKAZI

Watendaji

40. Watendaji katika Makao Makuu na Katika Mikoa na Wilaya watateuliwa ama na Mwenyekiti wa CHAMA au na Kamati Kuu ya CHAMA, kama inavyoonekana inafaa kwa mujibu wa Katiba ya CHAMA CHA MAPINDUZI.

Katibu Mkuu

41. Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi ambaye atateuliwa na Mwenyekiti wa CHAMA:—

(a) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Jumuiya ya Wafanyakazi na atafanya kazi zake chini ya uongozi wa Baraza Kuu la Jumuiya ya Wafanyakazi;

(b) Atakuwa na wajibu wa kuitisha mikutano yote ya vikao vya juu vya Jumuiya ya Wafanyakazi akishauriana na Mwenyekiti;

(c) Atatunza fedha na kumbukumbu za Jumuiya ya Wafanyakazi.

Naibu Katibu Mkuu

42.—(a) Kutakuwa na Naibu Wawili wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa CHAMA;

(b) Naibu wa Katibu Mkuu mmoja ataishi na kufanya kazi zake Tanzania Bara na Naibu mwingine wa Katibu Mkuu ataishi na kufanya kazi zake Tanzania Visiwani;

(c) Manaibu Katibu Mkuu watakuwa wasaidizi wakuu wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi kwa shughuli zote za Jumuiya hii Tanzania nzima.

SEHEMU YA TANO

MENGINEYO

Baraza la Wadhamini

43. Jumuiya ya Wafanyakazi itakuwa na uwezo wa kumiliki kwa niaba ya CHAMA mali inayoondosheka na isiyoondosheka na mali inayomilikiwa hivyo itakuwa chini ya uangaliz na usimamizi wa Baraza dogo la wadhamini la Jumuiya litakalokuwa chini ya Baraza la Wadhamini la CHAMA.

Kiwango cha Mikutano

44. Isipokuwa kama imeagizwa vingine katika Kanuni hizi kiwango cha Mikutano ya Vikao vyote vya Jumuiya ya Wafanyakazi, kitakuwa ni nusu ya Wajumbe walio na haki ya kuhudhuria katika kikao kinachohusika.

45. Katika maswala yanayohusu kubadilisha Kanuni za Jumuiya ya Wafanyakazi au jambo lingine lolote linalohusu kubadilishana utaratibu wowote wa kimsingi katika Mikutano Mikuu ya Jumuiya ya Wafanyakazi, uamuzi utakuwa kwa makubaliano ya theluthi mbili za Wajumbe kutoka Tanzania Visiwani na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Tanzania Bara. Uamuzi mwingine wowote wa vikao vya Jumuiya utafuata makubaliano ya jumla au wingi wa kura za Wajumbe waliohudhuria. Lakini katika shughuli zozote za uchaguzi wa viongozi kura zitakuwa kwa siri, isipokuwa kama imeagizwa vingine katika Kanuni hizi.

Nafasi zikiwa wazi

46. Wakati wowote kunapotokea nafasi wazi miongoni mwa viti vyovyote vya Jumuiya ya Wafanyakazi kikao kinachohusika kitajaza nafasi hiyo bila ya kuchelewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

47. Mfanyakazi mwanachama wa JUWATA anayetaka kujiuzulu kutoka katika Jumuiya ya Wafanyakazi atafanya hivyo kwa kuandika barua ya kujiuzulu na kupeleka kwa Katibu wa Tawi wa JUWATA. Kiongozi anayetaka kujiuzulu atafanya hivyo kwa kuandika barua na kuipeleka kwa Katibu wa kikao kilichomchagua au kama ni kiongozi aliyeteuliwa kupitia kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi. Kujiuzulu

48. Mjumbe yeyote wa kikao chochote kilichowekwa na Kanuni hizi, ataacha kuwa Mjumbe wa kikao hicho iwapo hatahudhuria Mikutano mitatu mfululizo ya kikao chake, isipokuwa kwa sababu zinazokubaliwa na kikao chenyewe. Mahudhuria katika Mikutano

49. Jumuiya ya Wafanyakazi itakuwa na mapato kutokana na kiingilio na ada za wanachama, ruzuku, shughuli mbali mbali za kiuchumi, misaada mbali mbali na fedha za michango iliyochangishwa kwa madhumuni yoyote maalum itakayokubaliwa na CHAMA. Mapato ya Jumuiya

50. Mapato na matumizi ya Jumuiya hii yatakaguliwa na kuangaliwa na Shirika la Taifa la ukaguzi wa fedna (Tanzania Audit Corporation). Ukaguzi wa Fedha

51. Mfanyakazi mwanachama wa JUWATA anayeomba nafasi ya uongozi wa aina yoyote katika Jumuiya ya Wafanyakazi hatakubaliwa kuwa ameshinda mpaka awe amepata zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa. Kiwango cha Kura katika Uchaguzi

52. Mwenyekiti wa vikao mbali mbali wa Jumuiya ya Wafanyakazi atakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyakazi aliyechaguliwa kwa mujibu wa kuendesha mikutano hiyo pale panapohusika kwa mujibu wa Kanuni hizi. Pamoja na Mwenyekiti, kiongozi yeyote wa Jumuiya ya Wafanyakazi kabla ya kuwa kiongozi lazima awe mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi na awe anatimiza masharti ya uongozi kwa kufuatana na Katiba ya Chama Cha Mapinduzi. Wenyeviti

53.—(a) Ngazi ya kwanza ya kutatua mgogoro baina ya Mwanachama au Mwanachama wa JUWATA na Mwajiri ni Kamati ya Tawi ya mahali pale pa kazi kama ipo, au Ofisi ya Wilaya kama mahali hapo hakuna Kamati ya Tawi. Mgogoro, Mwenendo na Nidhamu

(b) Ikiwa Kamati ya Tawi imeshindwa kumaliza mgogoro huo, itaupeleka kwa Katibu wa JUWATA wa Wilaya na itatoa taarifa kamili juu ya hatua zilizochukuliwa.

(c) Katibu wa JUWATA wa Wilaya akishirikiana na Kamati ya Usimamizi wa Majukumu ya Wilaya, ikilazimu ataingilia mgogoro huo. Ikiwa Wilaya itashindwa, Katibu wa JUWATA wa Wilaya atapeleka taarifa kamili kwa Katibu wa JUWATA wa Mkoa ambaye naye akishindwa atapeleka mgogoro huo kwa Katibu Mkuu wa JUWATA.

(d) Kwa vyovyote wafanyakazi wahusikao hawatasimamisha kazi zao au kutishia hivyo kabla ya kupata idhini ya Kamati ya Usimamizi wa Majukumu ya Baraza Kuu kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(e) Aidha Baraza Kuu halitakuwa na uwezo wa kuidhinisha au kushauri kitendo cha mgomo kuhusu mgogoro wowote wa kazi mpaka utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria itakapofuatwa kikamilifu, na iwapo kitendo cha aina hiyo, kitakubaliwa na Wafanyakazi wanaohusika kwa kura ya siri.

Passed in the National Assembly on the twenty-third day of October, 1979.

.....
Clerk of the National Assembly

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam—Tanzania